



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 JULAI, 2021 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 AGOSTI, 2021.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 JULAI, 2021.

Katika dekadhi hii, migandamizo mikubwa iliyopo Kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyoko Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhoofika. Hali hii iliendelea kuushikilia ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kuongeza mwendo kasi wa upepo hususan katika maeneo ya ukanda wa Pwani ya bahari ya Hindi. Joto la bahari katika eneo la pembe ya Kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi lilikua la chini kidogo ya wastani. Hali hii ilikua na mchango katika kusukumwa kwa hewa yenye ubaridi kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Joto la juu ya wastani lilikuwepo upande wa kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na kupunguza kasi ya upepo uvumao kutoka magharibi mwa misitu ya Kongo kuelekea maeneo ya Magharibi mwa nchi yetu. Kwa ujumla, mifumo ya hali ya hewa tajwa hapo juu, ilisababisha maeneo mengi ya nchi kuendelea kuwa makavu na yenye hali ya ubaridi ikiambatana na upepo wenye mwendo kasi wa wastani hadi mkali katika maeneo mengi ya nchi.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 JULAI, 2021.

Maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu na yenye ubaridi. Hata hivyo, vipindi vya mvua nyepesi vikiambatana na vipindi vya upepo wa wastani hadi mkali, mawimbi makubwa katika maeneo ya ukanda wa Pwani na katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini-mashariki.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01- 10 AGOSTI, 2021.

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 AGOST, 2021

Katika dekadhi hii ya 22, migandamizo mikubwa iliyopo Kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuushikilia ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika maeneo mengi ya nchi yetu na hivyo kuongeza mwendo kasi wa upepo katika maeneo mengi ya nchi.

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

Wakati huo huo, upepo wenye ubaridi unatarajiwa kuendelea kusukumwa kutokea kizio cha kusini kuelekea katika maeneo mengi ya nchi yetu. Hali hii inachagizwa na matarajio ya uwepo wa joto la bahari la chini kidogo ya wastani maeneo ya pembe ya Kusini ya kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi. Upande wa kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) joto la bahari linatarajiwa kuwa la juu ya wastani na hivyo kupunguza kasi ya upepo uvumao kutoka magharibi mwa misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi yetu na hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo haya. Kwa ujumla, mifumo tajwa ya hali ya hewa, inatarajiwa kusababisha maeneo mengi ya nchi kuendelea kuwa makavu na yenye hali ya ubaridi na upepo wenye mwendo kasi wa wastani hadi mkali katika maeneo mengi ya nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 AGOSTI, 2021.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Vipindi vifupi vya ngurumo za radi katika maeneo machache vinatarajiwa.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Hali ya ukavu na ubaridi kwa ujumla. Hata hivyo, vipindi vifupi vya mvua nyepesi katika maeneo ya miinuko vinatarajiwa.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Mvua nyepesi katika maeneo machache ikiambatana na hali ya ubaridi.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yakiambatana na hali ya ubaridi.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yakiambatana na hali ya ubaridi.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu yakiambatana na hali ya ubaridi.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yakiambatana na hali ya ubaridi.

Imetolewana; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd

S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz